JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Menejimenti ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 2483,
Dar es Salaam.

Kumb. Na. AC.260/333/012

8 Julai, 2011

WARAKA WA MAENDELEO YA UTUMISHI NA.1 WA MWAKA 2011

MUUNDO WA MAENDELEO YA UTUMISHI WA KADA CHINI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS

1. UTANGULIZI:

Hivi karibuni vyuo mbalimbali vimekuwa vikitoa mafunzo katika fani ya mazingira hapa nchini. Hata hivyo, imekuwa vigumu kwa Wahitimu wa fani hizo kupata ajira zinazoendena na taaluma zao katika Utumishi wa Umma kwa kuwa hakuna muundo wa maendeleo ya utumishi wa kada inayohusika na hifadhi ya Mazingira. Aidha, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (Sura 191), Changamoto na Maazimio yanayotokana na Mikataba mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa inayohusu usimamizi na hifadhi ya mazingira, imetoa msisitizo wa umuhimu wa kuanzishwa kwa kada hii.

Kwa misingi hii, muundo huu unaanzishwa ili kusaidia katika masuala ya ajira na maendeleo ya watumishi wa kada zinazohusika na usimamizi na hifadhi ya mazingira katika Utumishi wa Umma.

2. SIFA NA UTARATIBU WA KUAJIRIWA NA KUPANDISHWA VYEO:

Kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008, Kifungu 4.2, 4.3 na 4.4 kuajiriwa au kupanda daraja kutazingatia sifa za msingi zilizotajwa katika Miundo ya Utumishi, ujuzi, stadi na haiba na utendaji kazi mzuri wenye matokeo kwa kuzingatia vigezo vinavyoainishwa katika tathmini ya upimaji utendaji kazi kwa uwazi (OPRAS).

Aidha, upandishwaji vyeo utazingatia pamoja na mambo mengine, maendeleo ya kitaaluma (career development), urithishaji madaraka (succession plan), na kuwepo kwa nafasi na Ikama iliyoidhinishwa na kutengewa fedha.

3. NYONGEZA ZA MWAKA ZA MISHAHARA:

Nyongeza za mwaka za mishahara zitatolewa kwa kuzingatia utendaji mzuri wa kazi na kufikia malengo yanayopimika. Maafisa ambao watahudhuria mafunzo yasiyopungua mwaka mmoja wa mafunzo na kutunukiwa Shahada/Stashahada ya Uzamili (Postgraduate Diploma/Masters) katika fani ya kazi zao, watapewa nyongeza mbili za mshahara kuanzia tarehe wanapopata sifa hizo. Hata hivyo, nyongeza za mishahara zitakazotolewa hazipaswi kuvuka upeo wa juu (bar) wa ngazi ya mshahara aliyopo mtumishi.

4. MASHARTI YA KAZI:

Kada hii itakuwa chini ya masharti ya Kudumu na Malipo ya Pensheni kwa mujibu wa Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma sura 371 na Akiba ya Wafanyakazi Serikalini (GEPF).

5. NIDHAMU:

Mamlaka ya nidhamu kwa kada hii ni ile iliyotajwa katika Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 ya Utumishi wa Umma ikisomwa pamoja na Rekebisho lake Na. 9 la mwaka 2008, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, Toleo la Tatu (2009), Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 16 wa mwaka 1990 kulingana na cheo cha mhusika.

6. VYEO NA NGAZI ZA MISHAHARA:

Chini ya Muundo huu, vyeo na ngazi za mishahara zitakuwa kama ifuatavyo:-

NYONGEZA I – MUUNDO WA UTUMISHI WA MAAFISA MAZINGIRA (ENVIRONMENT OFFICERS)

Afisa Mazingira Daraja la II	TGS D
Afisa Mazingira Daraja la I	TGS E
Afisa Mazingira Mwandamizi	TGS F
Afisa Mazingira Mkuu Daraja la II	TGS G
Afisa Mazingira Mkuu Daraja la I	TGS H

7. TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA:

Muundo huu umejadiliwa na kukubaliwa na Baraza Kuu la Wafanyakazi Katika Utumishi wa Umma katika mkutano wake uliofanyika tarehe 21 - 22 Februari, 2011, na unaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2011. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itawajibika katika kuhakikisha kwamba Muundo huu unatumika ipasavyo. Aidha, Maafisa Masuuli wote wanapaswa kushughulikia ajira, maslahi na maendeleo ya watumishi wa kada hii waliopo katika Wizara/Idara zao kwa mujibu wa maelekezo ya Waraka huu.

GEORGE D. YAMBESI,
Katibu Mkuu (Utumishi)

MUUNDO WA UTUMISHI WA MAAFISA MAZINGIRA (ENVIRONMENT OFFICERS)

UTARATIBU WA KUAJIRIWA NA KUPANDISHWA VYEO:

1. Afisa Mazingira Daraja la II (TGS D)

(a) *Sifa za kuingilia moja kwa moja:*

Kuajiriwa wahitimu wenye Shahada ya kwanza ya Sayansi/Sanaa yenye mwelekeo wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira katika moja ya fani zifuatazo; "*Geography and Environmental Studies, Aquatic Environmental Science and Conservation, Environmental Science and Management, Environmental Laboratory Science Technology, Environmental Planning and Management*" au sifa zinazolingana na hizo kutoka Vyuo vinavyotambulika na Serikali.

(b) *Sifa za kuingilia waliomo kazini:*

Kubadilishwa vyeo watumishi wa kada nyingine ambao wamejipatia sifa zilizotajwa katika kifungu cha 1 (a) hapo juu.

(c) *Kazi za kufanya:*

(i) Kukusanya Takwimu na Taarifa mbalimbali zinazohusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira.

(ii) Kutoa (disseminate) elimu ya Hifadhi ya Mazingira kwa wadau mbalimbali.

(iii) Kushiriki katika kuandaa mpango wa kazi na bajeti.

(iv) Kushiriki katika tafiti zinazohusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira.

(v) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Sheria zi - husiana na usimamizi wa Mazingira.

(vi) Kufuatilia na kuainisha maeneo yanayopaswa kuhifadhiwa.

(vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa kulingana na uwezo na taaluma yake.

2. Afisa Mazingira Daraja la I (TGS E)

(a) *Sifa za kuingilia moja kwa moja:*

Kuajiriwa wahitimu wenye Shahada ya kwanza ya Sayansi/Sanaa yenye mwelekeo wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira katika moja ya fani zifuatazo; "*Geography and Environmental Studies, Aquatic Environmental Science and Conservation, Environmental Science and Management, Environmental Laboratory Science Technology, Environmental Planning and Management*" au sifa zinazoelekeana na hizo kutoka Vyuo vinavyotambulika na Serikali wenye uzoefu wa kazi za usimamizi wa mazingira usiopungua miaka mitatu.

(b) *Sifa za kuingilia waliomo kazini:*

Kupandishwa cheo Maafisa Mazingira Daraja la II, wenye utendaji mzuri wa kazi kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008 na wenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

(c) *Kazi za kufanya:*

(i) Kukusanya na kuchambua taarifa mbalimbali zinazohusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira.

(ii) Kutoa elimu kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Mazingira.

(iii) Kufanya tafiti kuhusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira.

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Sheria nyingine zinazohusiana na Usimamizi na Hifadhi ya mazingira.

(v) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa kulingana na uwezo na taaluma yake.

3. **Afisa Mazingira Mwandamizi (TGS F)**

(a) *Sifa za kuingilia moja kwa moja:*

Kuajiriwa wahitimu wenye Shahada ya kwanza ya Sayansi/Sanaa yenye mwelekeo wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira katika moja ya fani zifuatazo; "*Geography and Environmental Studies, Aquatic Environmental Science and Conservation, Environmental Science and Management, Environmental Laboratory Science Technology, Environmental Planning and Management*" au sifa zinazoelekeana na hizo kutoka Vyuo vinavyotambulika na Serikali wenye uzoefu wa kazi za Usimamizi na Hifadhi ya mazingira usiopungua miaka sita.

(b) *Sifa za kuingilia waliomo kazini:*

Kupandishwa cheo Maafisa Mazingira Daraja la I ambao wamepata sifa iliyotajwa katika kifungu cha 3 (a) hapo juu, wenye utendaji mzuri wa kazi kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008 na wenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

(c) *Kazi za kufanya:*

(i) Kupitia na kushauri kuhusu utekelezaji wa Sera, Sheria ya Mazingira na Miongozo na Mikakati mbalimbali kuhusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira.

(ii) Kuandaa Taarifa ya Hali ya Mazingira nchini (State of the Environment Report).

(iii) Kupitia na kushauri kuhusu Taarifa za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (Environmental Impact Assessment) na Mpango-mkakati wa Tathmini ya Mazingira (Strategic environmental Assessment).

(iv) Kubuni na kupendekeza miradi mbalimbali kuhusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira.

(v) Kuandaa na kuratibu utekelezaji wa mikakati ya matumizi salama ya tekinolojia ya kisasa (biosafety).

(vi) Kufanya tathmini ya maeneo yaliyoathirika kutokana na shughuli za uchumi zisizo endelevu (kama uchimbaji madini, kilimo, ujenzi, ufugaji, n.k.).

(vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa kulingana na uwezo na taaluma yake.

4. **Afisa Mazingira Mkuu Daraja la II (TGS G)**

(a) *Sifa za kuingilia moja kwa moja:*

Kuajiriwa wahitimu wenye Shahada/Stashahada ya Uzamili ya sayansi/sanaa yenye mwelekeo wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira katika moja ya fani zifuatazo; "*Geography and Environmental Studies, Aquatic Environmental Science and Conservation, Environmental Science and Management, Environmental Laboratory Science Technology, Environmental Planning and Management*" au sifa zinazoelekeana na hizo kutoka Vyuo vinavyotambulika na Serikali wenye uzoefu wa kazi za usimamizi wa mazingira usiopungua miaka tisa.

(b) *Sifa za kuingilia waliomo kazini:*

Kupandishwa cheo Maafisa Mazingira Waandamizi ambao wamepata sifa iliyotajwa katika kifungu cha 4 (a) hapo juu, wenye utendaji mzuri wa kazi kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008 na wenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

(c) *Kazi za kufanya:*

(i) Kusimamia matumizi ya rasilimali mbalimbali za hifadhi ya mazingira.

(ii) Kuchambua na kusambaza takwimu za hifadhi ya mazingira.

(iii) Kufuatilia na kushauri utekelezaji wa Sera na Sheria nyingine zinazohusiana na Usimamizi wa Mazingira.

(iv) Kufuatilia na kushauri kuhusu utekelezaji wa Mikataba na Maazimio mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa kuhusu Usimamizi na Hifadhi ya mazingira.

(v) Kupendekeza miradi ya hifadhi ya Mazingira.

(vi) Kupitia na kushauri kuhusu Taarifa ya Hali ya Mazingira nchini (State of the Environment Report).

(vii) Kupitia na kutoa mapendekezo kuhusu Taarifa za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (Environmental Impact Assessment) na Mpango-mkakati wa Tathmini ya Mazingira (Strategic environmental Assessment).

(viii) Kuratibu miradi mbalimbali inayohusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira.

(ix) Kubainisha na kupendekeza masuala ya mazingira ambayo yanapaswa kuhuishwa katika mipango ya kisekta.

(x) Kuratibu utekelezaji wa mikakati ya matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa (biosafety).

5. **Afisa Mazingira Mkuu Daraja la I (TGS H)**

(a) *Sifa za kuingilia moja kwa moja:*

Kuajiriwa wahitimu wenye Shahada/Stashahada ya Uzamili ya Sayansi/Sanaa yenye mwelekeo wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira katika moja ya fani zifuatazo; "*Geography and Environmental Studies, Aquatic Environmental Science and Conservation, Environmental Science and Management, Environmental Laboratory Science Technology, Environmental Planning and Management*" au sifa zinazoelekeana na hizo kutoka Vyuo vinavyotambulika na Serikali wenye uzoefu wa kazi za usimamizi wa mazingira usiopungua miaka kumi na mbili.

(b) *Sifa za kuingilia waliomo kazini:*

Kupandishwa cheo Maafisa Mazingira Wakuu Daraja la II ambao wamepata sifa iliyotajwa katika kifungu cha 5 (a) hapo juu, wenye utendaji mzuri wa kazi kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008 na wenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

(c) *Kazi za kufanya*

(i) Kutoa mapendekezo kuhusu utekelezaji wa Sera na Sheria nyingine zinazohusiana na usimamizi wa mazingira.

(ii) Kutoa ushauri kuhusu utekelezaji wa Mikataba na Maazimio mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa kuhusu usimamizi wa Mazingira.

(iii) Kuandaa michanganuo ya miradi ya hifadhi ya mazingira.

(iv) Kupitia Taarifa ya Hali ya Mazingira nchini *(State of the Environment Report)* na kutoa ushauri.

(v) Kupitia Taarifa za Tathmini ya Athari kwa Mazingira *(Environmental Impact Assessment)* na Mpango-mkakati wa Tathmini ya Mazingira *(Strategic environmental Assessment)* na kutoa ushauri.

(vi) Kuratibu miradi mbalimbali inayohusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira.

(vii) Kubainisha na kupendekeza masuala ya mazingira yanayopaswa kuhuishwa katika mipango ya kisekta.

(viii) Kusimamia utekelezaji wa mikakati ya matumizi salama ya tekinolojia ya kisasa (biosafety).

(ix) Kutoa ushauri kuhusu maeneo yaliyoathirika kutokana na shughuli za uchumi zisizo endelevu (kama uchimbaji madini, kilimo, ujenzi, ufugaji, n.k.).

(x) Kuratibu maandalizi ya bajeti ya miradi ya Idara.

(xi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa kulingana na uwezo na taaluma yake.